TANGAZO LA SERIKALI Na. 1027 la tarehe 11/12/2020

(SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA)

(SURA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu 7 (1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO ZA HALMASHAURI YA WILAYA NANYUMBU ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi na Maegesho za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu za mwaka 2020.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi itatumika katika eneo lote lililopo chini ya Halmashauri.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yoyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu;.

"maegesho" maana yake ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuegesha magari isipokuwa maeneo yaliyo katika hifadhi za barabara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu na pamoja na Afisa yoyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki" maana yake ni mmiliki wa gari na ni pamoja na dereva;

''ushuru'' maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa huduma inayotolewa na Halmashauri au katika eneo la Halmashauri;

''Wakala'' maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi.

Kuanzishwa kwa stendi

4.-(1) Halmashauri itaanzisha maeneo maalum yatakayotumika kama stendi kwa ajili ya huduma za magari ya abiria au mizigo.

(2) Mmiliki wa gari la abiria au mizigo ambaye, bila sababu ya msingi, atapakia au kushusha mizigo, nje ya eneo lililotengwa kwa ajili ya kupakia au kushusha abiria au mizigo atakuwa ametenda kosa.

Ushuru

5. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa ajili ya magari ya abiria na mizigo kama ulivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru wa stendi utalipwa wakati gari linapotoka au kuingia stendi kuendelea na safari yake

(3) Ushuru wa stendi utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki.

(4) Masharti ya kifungu hiki yatatumika pia kwa magari binafsi, pikipiki za magurudumu matatu, pikipiki za magurudumu mawili na mikokoteni.

Wajibu wa kuingia stendi

6.-(1) Kila mmiliki wa gari la abiria au mizigo linalotoka au kwenda mikoani au ndani ya eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa kuhakikisha gari lake linaingia katika stendi ya abiria au mizigo kwa kadri itakavyokuwa.

(2) Magari yote ya abiria yatatakiwa kuwa na kibao kinachoonesha mahali linapotoka na linakoelekea.

(3) Mmiliki atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kulipa ushuru

7.-(1) Kila mmiliki atakuwa na wajibu wa kulipa ushuru wa stendi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mmiliki atakayeshindwa kulipa ushuru wa stendi atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), Halmashauri inaweza kukamata na kushukilia gari ambalo mmiliki wake ameshindwa kulipa ushuru wa stendi hadi hapo ushuru pamoja na gharama za kushikilia gari hilo zitakapolipwa.

(4) Halmashauri haitwajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya ushuru isipokuwa kama hasara hiyo itasababishwa na uzembe wa Halmashauri, Mtumishi wa Halmashauri au Wakala

Maegesho

8.-(1) Halmashauri inaweza kutenga maeneo ya maegesho ya vyombo vya usafiri ambayo yatalipiwa ushuru ulioainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Masharti ya kifungu cha 6 yatatumika katika kusimamia ulipaji wa ushuru katika maegesho.

Masuala yasiyoruhusiwa

9.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:

(a) bila sababu za msingi kufanya matengenezo ya gari katika eneo la stendi au maegesho;
(b) kuosha gari katika eneo la stendi au maegesho;
(c) kuziba njia ya stendi au maegesho ya magari; au
(d) kuegesha gari katika eneo lisirohusiwa ndani ya stendi au maegesho

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi,

Adhabu

10. Mtu yoyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hizi atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne, au adhabu zote mbili kwa pamoja yani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa iwapo mkosaji atakiri kwa hiyari yake kwa maandishi na kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kutimiza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi na kulipa kiasi cha shilingi shilingi laki mbili.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5(1))*

USHURU WA STENDI

| Na. | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI | KIASI KWA SIKU MOJA |
|---|---|---|
| 1. | Basi la abiria zaidi ya 40 | 2,000/= |
| 2. | Basi la abiria chini ya 40 | 1,500/= |
| 3. | Basi la abiria chini ya 20 | 1,000/= |
| 4. | Taxi (Taxi Cabs) | 1,000/= |
| 5. | Magari Binafsi | 1,000/= |
| 6. | Gari dogo la mizigo | 1,000/= |
| 7. | Gari kubwa la mizigo | 2,000/= |
| 8. | Pikipiki Magurudumu Matatu | 1,000/= |
| 9. | Pikipiki Magurudumu Mawili | 500/= |
| 10. | Mkokoteni | 300/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

MAENEO YA MAEGESHO

| a. | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI | KIASI KWA SIKU MOJA |
|---|---|---|
| 1. | Basi la abiria zaidi ya 40 | 10,000/= |
| 2. | Basi la abiria chini ya 40 | 5,000/= |
| 3. | Basi la abiria chini ya 20 | 2,000/= |
| 4. | Taxi | 1,500/= |
| 5. | Magari Binafsi | 1,000/= |
| 6. | Gari dogo la mizigo | 5,000/= |
| 7. | Gari kubwa la mizigo | 10,000/= |
| 8. | Pikipiki Magurudumu Matatu | 1,000/= |
| 9. | Pikipiki Magurudumu Mawili | 500/= |
| 10. | Mkokoteni | 300/= |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi…………..………………..……………….. kwa hiari yangu mwenyewe nakiri mbele ya……….………... Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kwamba mnamo tarehe……… ya mwezi wa………………….mwaka………. nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ……………….. cha Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi na Maegesho za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu za Mwaka 2020.

Nipo tayari kulipa shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu mwenyewe kadri ya ufahamu wangu.

Leo Tarehe………………………………..ya Mwezi…………………Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu iligongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 4/2/2020 n iligongwa mbele ya:-

PONSIAN KAZEE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Nanyumbu*

AHMAD B. MCHOPA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Nanyumbu*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
28 Septemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*